

# WANAWAKE KAMA WAANGALIZI WA MBEGU

**W**anawake wamekuwa wazalishaji wa mazao na wazalishaji wa mbegu tangu kuanza kwa kilimo zama za kale. Katika jamii nyingi za Kiafrika vijijini, wanawake wamekuwa waangalizi wa mifumo ya mbegu. Wakichagua na kuhifadhi mbegu kutoka kwenye mavuno na kuziendeleza, kubadilishana na kuzitumia tena kwenye kupanda, wanawake hutekeleza wajibu muhimu katika kuhakikisha uhakika wa chakula, ustahimilivu na uthabiti wa mazao yao na uanuwai wa mbegu zao.



Wanawake hujishughulisha na mazao yaliyo na thamani ndogo kibiashara ambayo ni muhimu kwa lishe ya kaya na uhakika wa chakula. Mazao haya ni pamoja na mtama, ulezi, karanga, muhogo, kunde na mboga za majani kama vile mchicha, mung'unye, maboga, kisamvu na mtunguja.

Hata hivyo, wakulima wanaposhinikizwa kupanda mbegu za biashara kutoka sekta rasmi, wanawake hushindwa kuendelea na desturi yao ya miaka mingi ya kuchagua na kuhifadhi mbegu zao. Wanatarajiwa wanunue mbegu zilizothibitishwa ambazo ni ghali kila mwaka na kupanda mbegu chotara katika kilimo cha zao moja. Aidha, wanalazimika kununua madawa ya kilimo na mbolea ambavyo ni ghali na hutumika pamoja na mbegu iliyothibitishwa. Hali hii husababisha madeni na utegemezi, na hudhoofisha kwa kiwango kikubwa wajibu wa wanawake kama waangalizi wa mbegu.

